



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI



TANGAZO

MPANGO WA UTAMBUZI NA URASIMISHAJI UJUZI

Je wewe ni kijana mwenye umri usiozidi miaka 45?

Je ni fundi lakini ulipata ujuzi bila kupitia chuoni na hivyo hauna cheti?

Je una uzoefu kwenye fani yako usiopungua miaka mitano?

Je ungependa ujuzi wako utambuliwe na kurasimishwa ili upewe cheti kulingana na ujuzi wako?

Kama ndivyo, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kwa kushirikiana na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) wanaendesha **Awamu ya Nne ya Mpango wa Kutathmini na Kurasimisha Ujuzi Uliopatikana Nje ya Mfumo Rasmi wa Mafunzo**.

Katika Mpango huu, unayo fursa ya kufanyiwa tathmini ya ujuzi wako, kupewa mafunzo ili kuziba mapungufu, kisha kutunukiwa cheti.

Jumla ya fani kumi zitahusika katika awamu hii. Fani hizo ni Uashi, Useremala, Ufundi Magari (makenika), Upishi na U hudumu wa Hoteli, Baa na Migahawa. Fani zingine ni Ufundi bomba, Unyooshaji bodi za magari, Umeme wa majumbani, Ufundi Cherehani na Uchomeleaji vyuma.

Ikiwa unakidhi masharti yaliyotajwa hapo juu, fika au wasiliana na sehemu zifuatazo ili ujiandikishe na kuchukua fomu :

1. Ofisi za Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa au Majiji, nchini kote
2. Vyuo vyote vya VETA nchini kote.
3. Tovuti ya VETA ambayo ni www.veta.go.tz na
4. Tovuti ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo ni www.pmo.go.tz

Maombi yawasilishwe kuanzia tarehe 19 Januari, 2022 hadi tarehe 18 Februari, 2022.

Watakaokidhi sifa, vigezo na masharti watajulishwa kwa ajili ya usaili utakaoanza mwezi Februari 2022.

Mchakato wote wa tathmini na urasimishaji wa ujuzi utagharamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira, na Wenye Ulemavu. Washiriki hawatalipia gharama yoyote.

Imetolewa na Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Elimu na Mafunzo Ya Ufundi Stadi (VETA)

